



SNCOOP



KANUNI 8 ZA MSINGI YA UONGOZI BORA NDANI YA VIKUNDI VYA MAENDELEO KIJIJINI

Kanuni zinazo onesha uongozi bora ndani ya kamati za vikundi vya maendeleo kijijini :



1. Kuwepo kwa sheriya zinazoongoza kikundi (Statuts ya kikundi, kanuni za wa fanyakazi ao R.O.I)



2. Udemocrasia : mwanamemba moja sauti moja ; wanamemba wote wana haki sawa.



3. Uwazi katika uongozi ama transparence : kukuwa wazi bila ujanja katika uongozi inasaidiya wanamemba kuelewa namnagani vi kundi vinaendelea ku pitiya ripoti iliyo wazi.



4. Uwajibu ama kutoa ripoti ya madaraka ulipewa / redevabilité : uwajibu ni kanuni inayolomba mutu aliye pewa uongozi atowe ripoti kwa niaba ya walio chini ya madaraka yake.

Katika mupango ya vikundi vya ma maendeleo kwenye kijiji, uwajibu inaendeshwa kulingana na mupango ya uogoi, kuanziya juu hadi kwa wafanyakazi wa chini.



5. Uwezo ya kuleta mabadiliko bora: Kisha kuchaguliwa ama kupewa kazi, wanamemba wa kikundi cha maendeleo kwenye kijiji wanahitaji kucanga mawazo ya mupya na kuweka mbinu mbalimbali ya kusaidiya kikundi ao shirika lao liende mbele waki boresha zaidi utendaji piya mabadiliko yenyi kuonekana.

Kiongozi analazimishwa kutumia pesa za kikundi kwa faida ya watu wote, katika kusudi ya kutimiza ma lengo za kikundi apana ju ya haja zake mwenyewe.



6. Usawa : Usawa ndani ya mambo ya uongozi inasaidiya kupatanisha watu wote katika kundi ingawaje maoni yao yako tafauti. Inasaidiya piya kazi za kikundi kuendelea mbele ingawaje shida mbalimbali zenye kuzuiya maendeleo, piya inasaidiya watu wote kufanya kazi kila mutu kwa kiwango yake bila ubaguzi.



7. Kuhusisha wengine bila kubaguwa wamoja : Kwakuheshimu kanuni hii, itasaidiya pia mukubwa wa muungano (kikundi) kuheshimu sheriya zilizo wekwa na kuepuka kutumiya madaraka munjiya yenye hai fai (ama njiya za giza)



8. Kujitoleya : Kwa kujikataliya, kiongozi atajikaza kutumikisha tu faida zenye kikundi ama shirika inamupatiya kulingana na sheriya na kulingana na makubaliano ya mapatano ama contrat aliwezaka signer.